**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TISA

## KIKAO CHA TISA

**17 NOVEMBA, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA TISA

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 17 NOVEMBA, 2017

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI MKUU:**

Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017 *[The Drug Control and Enforcement (Amendment) Bill, 2017].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI:**

Maoni ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017 *[The Drug Control and Enforcement (Amendment) Bill, 2017].*

## MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU:

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017 *[The Drug Control and Enforcement (Amendment) Bill, 2017]*.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 107. MHESHIMIWA DKT. DALALY PETER KAFUMU (IGUNGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Zaidi ya asilimia 70 ya eneo la Jimbo la Igunga lilikuwa limefunikwa na maji ya Ziwa Victoria lakini baada ya Ziwa hilo kukauka eneo hilo limebaki kuwa ni Mbuga inayojaa maji wakati wa masika hivyo kufanya ujenzi wa barabara za Vijiji kuwa wa gharama kubwa sana na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga haimudu gharama hizo:-

Je, kwa nini Serikali isiandae mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara za Vijijini katika Wilaya ya Igunga na Wilaya nyingine nchini zenye tatizo kama hili.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

**108. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Tatizo la uhaba wa Watumishi Idara ya Afya Urambo linaathiri sana utoaji wa huduma za afya kwa Wananchi:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura kuliondoa tatizo hilo;

(b) Je, Serikali inaweza kuchukua Vijana wa Urambo na kuwapeleka Vyuoni kusoma kwa makubaliano ya kurudi kufanya kazi Urambo.

**109. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASSIN CHIKAMBO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Ukosefu wa nyumba za Walimu Vijijini kunafanya Walimu kuhama kwenye maeneo hayo na kusababisha upungufu mkubwa wa Walimu. Aidha, Halmashauri nyingi zikiwemo za Mkoa wa Ruvuma hazina uwezo wa kujenga nyumba za Walimu kwa kutumia fedha za ndani:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga nyumba za Walimu wa Shule za Msingi Vijijini ili kuwawekea mazingira rafiki ya kufanya kazi.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**110. MHESHIMIWA GODBLESS JONATHAN LEMA (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Kukosekana kwa mpango madhubuti wa mipango Miji pamoja na gharama kubwa za ujenzi zinazosababishwa na kodi kubwa katika vifaa vya ujenzi kumefanya Wananchi kujenga kiholela:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali isiondoe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vyote vya ujenzi;

(b) Shirika la Nyumba la Taifa linajenga nyumba bora za makazi na biashara; Je, ni kwa nini Serikali isiondoe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyumba za Shirika hilo ili ziwe za bei nafuu.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**111. MHESHIMIWA HAMIDU HASSAN BOBALI (MCHINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Sekta ya Uvuvi bado haijatumika kikamilifu kulipatia Taifa pato na kuwaondoa Watanzania hususan Wavuvi katika dimbwi la umaskini.

(a) Je, ni lini Serikali itaweka jitihada za kusaidia Wavuvi hasa wale wanaojihusisha na Uvuvi wa Bahari Kuu;

(b) Je, ni lini Serikali itatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Wavuvi wadogo wadogo ili waweze kuvua katika Bahari Kuu.

**112. MHESHIMIWA HASNA SUDI KATUNDA MWILIMA (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Shughuli kubwa za kiuchumi kwa Wananchi wa ukanda wa Ziwa Tanganyika ni Uvuvi lakini nyavu zao zimekuwa zikikamatwa na kuchomwa moto:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia Wavuvi hao nyenzo au vifaa vya kisasa vya Uvuvi.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**113. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kwa muda mrefu chanzo cha maji cha Ruvu Chini na Ruvu Juu kimekuwa chanzo

PARLIAMENT OF TANZANIA BUNGE LA TANZANIA

pekee cha maji katika Mkoa wa Pwani. Lakini kimsingi chanzo hicho hakitoshelezi mahitaji na hivyo kushindwa kumaliza tatizo la maji:-

Je, ni lini Serikali itatumia chanzo cha maji cha Mto Rufiji kuwapatia maji safi na salama Wananchi hususan wa Wilaya ya Rufiji, Kibiti, Mkuranga na Kisarawe.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**114. MHESHIMIWA NURU AWADH BAFADHILI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Askari Polisi wengi katika Jiji la Tanga wanaishi uraiani ambapo ni kinyume cha maadili kutokana na ukosefu wa nyumba za kuishi katika kambi zao:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga upya nyumba za Askari hao;

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwajengea nyumba za ghorofa Askari wa Kambi za Chumbageni, Mabawa na Madina Msambweni ili ziweze kuwaweka Askari wengi katika eneo moja kama ilivyo Kilwa Road Dar es Salaam.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## WIZARA YA NISHATI:

**115. MHESHIMIWA OMARY TEBWETA MGUMBA (MOROGORO KUSINI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Vijiji 17 pekee kati ya Vijiji 64 ndivyo vilivyopata umeme katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki na ni Vijiji 7 tu vya Ludewa, Mtego wa Simba, Kidugalo, Lung'ala, Mangala, Tumanguo na Kinonko vilivyo katika orodha ya kupatiwa umeme katika REA III awamu ya kwanza ya mwaka 2017/2018:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji 47 vilivyosalia.

## WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

**116. MHESHIMIWA SAED AHMED KUBENEA (UBUNGO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Serikali iliingia ubia na Kampuni kutoka Jamhuri ya Watu wa China ya kumiliki na kukiendesha Kiwanda cha Nguo cha Urafiki kilichoko Ubungo Jijini Dar es Salaam lakini Mbia huyo ameshindwa kutoa mtaji wa kuendesha Kiwanda hicho:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kuwa Mbia huyo anaweka mtaji wa kutosha wa kukiendesha Kiwanda hicho;

(b) Je, kwa nini Serikali inafikia maamuzi ya kukibinafsisha Kiwanda cha Umma kwa mtu ambaye hana mtaji.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**117. MHESHIMIWA HALIMA ABDALLAH BULEMBO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Kumekuwa na upandaji holela wa gharama za pango kwa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC):-

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kudhibiti upandaji holela wa pango ambao unaathiri Wananchi wengi kutokana na kipato chao.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**118. MHESHIMIWA KEMIREMBE JULIUS LWOTA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini ujenzi wa daraja la Kigongo Busisi utaanza.

**119. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu za mkononi katika Kata za Jimbo la Same Magharibi hususani Kata za Msindo, Mshewa, Mhuzi, Vumari, Vuudee, Tae, Suji, Gavao, Saweni na Ruvu Jiungeni.

**120. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Mkoa wa Singida kwa sasa ni Mkoa wa kimkakati hasa kufuatia kazi ya kuleta Makao Makuu Dodoma:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha Mkoa huo unapata Uwanja wa Ndege hasa kutokana na umuhimu wake.

## VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Kwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2017 *[The Written Laws (Miscelleneous Amendments) (No. 5) Bill, 2017].*

Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2017 *[The Public Service Security Fund, Bill, 2017].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Mwaka 2017 *[The Wildlife Conservation (Amendment) Bill, 2017].*

## VII. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017 *[The Drug Control and Enforcement (Amendment) Bill, 2017].*

## V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

## VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE :

**WAZIRI MKUU**

## VII. WIMBO WA TAIFA:

**DODOMA** **S.N. KAGAIGAI**
**17 NOVEMBA, 2017** **KATIBU WA BUNGE**